

Kama kituo cha afya ya akili ya jamii, sisi katika Kituo cha Afya ya Akili cha Denver tunajua kuwa sauti ya kila mtu ni muhimu. Kupiga kura katika uchaguzi ni njia moja nzuri ya kufanya sauti yako isikilikane. Unapo chaguwa kura, unaathiri maamuzi muhimu ambayo yana badilisha maisha yetu ya kila siku.

Tunataka kukuunga mkono katika kujiandikisha juu ya uchaguzi ikiwa unataka kushiriki katika uchaguzi wa mwaka huu.

### **Ginsi ya Kujiandikisha juu uchaguzi (au Sasisha Usajili wako):**

Kuna njia tatu za kujiandikisha juu uchaguzi:

1. **Mtandaoni (Ku internet):** Ikiwa una kitambulisho au Kitambulisho cha Dereva wa Jimbo la Colorado, unaweza [kujiandikisha juu uchaguzi ku internet hapa](#)

Tarehe ya mwisho ya kujiandikisha ku internet: Oktoba 25, 2021

2. **Kwa Mtu Pekee:** Unaweza kujiandikisha juu ya uchaguzi na kuchaguwa kibinafsi katika moja ya fasi huko Denver kuanzia katikati ya Oktoba (mwanzo ya hizi tarehe zitaangaliwa ku internet). [Kitambulisho hiyi](#) inaonyesha maeneo yote ya usajili wa mtu na mtu katika Denver.

Mwisho wa kujiandikisha wa mtuu pekee: Novemba 2, 2021 na 7PM (mangaribi) (siku ya uchaguzi)

3. **Kwa barua:** Ikiwa hauna kitambulisho ya Colorado au Kitambulisho au unataka kujiandikisha kwa barua, unaweza kuchapisha na kujaza hiyi [Kartasi ya kujiandikisha juu uchaguzi wa Colorado](#). Kisha tuma barua ao uipeleke we mwenyewe pa:

Colorado Department of State

Elections Division

1700 Broadway, Suite 200

Denver, CO 80290

ao

Denver Elections Division

200 W. 14<sup>th</sup> Ave.

Suite 100

Denver, CO 80204

ao fax it ku: 303-869-4861

Tarehe ya mwisho ya kujiandikisha ya Karatasi: Karatasi lazima zipokelewe katika ofisi ya uchaguzi ifikapo siku ya kwanza, Oktoba 26, 2020. Hakikisha kutuma au kuacha karatasi yako haraka iwezekanavyo ili kuhakikisha inafika tarehe ya mwisho. Ukikosa tarehe hii ya mwisho, hautapokea kura kwa barua, lakini bado unaweza chaguwa kibinafsi katika kituo cha huduma ya uchaguzi na kituo cha uchaguzi (tazama hapa chini). Unaweza kuangalia hali yako ya kujiandikisha na kupata majibu ya maswali ya kawaida kwenye [Katibu wa Jimbo la Colorado](#).

### **Maswali:**

- Ikiwa una maswali yoyote kuhusu kujiandikisha, tafazali wasiliana na Katibu wa Jimbo la Colorado: 303-894-2200 ao [elections@sos.state.co.us](mailto:elections@sos.state.co.us).

### **Jinsi ya kuchaguwa ( Ukisha maliza kujiandikisha):**

Katika Colorado, tuna njia tatu za kuchaguwa:

1. **Barua:** Kuanzia Oktoba 8, kila mtu aliyeandikishwa kuchaguwa atapokea kura kwa barua. Mara tu unapopokea kura yako, unaweza kujijaza, ukitia muhuri wako ao saini na kuipeleka.  
  
AO
2. **Kuacha:** Kurudisha kura yako iliyokamilishwa kwa sanduku zozote za [kura za zinafunguliwa saa 24](#) huko DenverAO
3. **Kwa Mtu Pekee:** Kuanzia Oktoba 18, unaweza chaguwa kibinafsi katika kituo chochote cha huduma ya wapigakura na vituo vya uchaguzi karibu na Denver. [Kitambulisho hii](#) inaonyesha eneo la vituo vya uchaguzi huko Denver.

## **Matatizo zinazowezekana & ginsi ya kutatua:**

Kujiandikisha juu ya uchaguzi na kuchaguwa huko Colorado imeundwa kupatikana kwa kila mtu. Hata hivyo, matatizo zingine zinaweza kutokea, pamoja na:

- Umeshindwa Kupokea Barua kwa Anwani ya Nyumbani  
*Watu ambao hawawezi kupokea barua kwenye anwani ya nyumbani, hawana nyumba ya kweli, au wanakabiliwa na ukosefu wa makaaji wanaweza kutumia anwani yoyote ambayo yenye hurejea kwao mara kwa mara. Hii inaweza kujumuisha makao ya wasio na makaaji, mtoa huduma asiye na makaaji, anwani ya biashara, au eneo lingine lolote la mahali.*
- Usafirishaji kwenda Kituo cha Kuchaguwa au Sanduku la kutia kartasi ya uchaguzi  
*Kwa ratiba za usafiri, maswali ya njia na nauli iliyopunguzwa, unaweza kupiga simu RTD at [303 299-6000](tel:3032996000) kwa msaada wa kutafuta na kupanga ginsi ya usafirishaji, unaweza kupiga simu kwa Baraza la Uhamaji na Upataji wa Mkoa wa Denver ku 303-243-3113 or go to: <https://www.drmac-co.org/>*
- Kununuwa Stamps  
*Posta ya uchaguzi ni senti 71, au stamps mbili za "forever". Kura bila stamps bado zitawasilishwa na kuhesabiwa.*
- Kucheleweshwa kwa Huduma ya Posta  
*Huduma ya Posta ya Merika (USPS) inakabiliwa na ucheleweshaji ambao unaweza tuma inachukua muda mrefu kabla ya kuchaguwa kufika baada ya kuipeleka. Hakikisha kutuma kura yako ya uchaguzi haraka iwezekanavyo ili ifike kabla ya Siku ya Uchaguzi (Novemba 2).*

## **Kwa Msaada Zaidi:**

Tafadhali wasiliana na timu yako ya matibabu kwa usaidizi wa kujiandikisha juu ya uchaguzi. Tuko hapa kukusaidia.